

## MSAADA WA KISHERIA

### 6.0 HITIMISHO

Izangaitwe kuwa cheti cha kuzaliwa sio uthibitisho wa uraia bali ni uthibitisho wa tarehe na mahali pa kuzaliwa. Suala la uraia linashughulikiwa na sheria za urai na uhamiaji.

Kwa Maoni, wasiliana na Tume  
kupitia anuni ifuatayo :

Katibu Mtendaji,  
Tume ya kurekebisha Sheria  
Tanzania ,

Jengo la Taaluma Na. 1,  
Barabara ya Mkalama  
S.L. P 1718  
DODOMA  
TANZANIA

Barua pepe: [lrct@lrct.go.tz](mailto:lrct@lrct.go.tz)  
Tovuti: [www.lrct.go.tz](http://www.lrct.go.tz)

JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA



## USAJILI WA VIZAZI

### 1.0 UTANGULIZI

Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (Tume) ilianzishwa mwaka 1980 kwa Sheria ya Tume Kwa mujibu wa sheria hii pamoja na majukumu mengine, Tume ina majukumu ya kufanya mapitio na kutathmini utekelezaji wa sheria zote za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kuziwezesha sheria hizo kuendana na mabadiliko yanayotokea katika nyanja za kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiteknolojia.

Katika kutekeleza jukumu hili, mwaka 2017 Tume ilifanya mapitio ya sheria zinazohusu usajili wa matukio muhimu ya binadamu.

### 2.0 SHERIA YA USAJILI WA VIZAZI NA VIFO, SURA 108

Kwa mujibu wa Sheria, usajili wa vizazi ni lazima na mtu yeyote aliyezaliwa Tanzania Bara anastahili kupata cheti cha kuzaliwa bila kujali umri wala jinsi. Baba au mama, na kama hawapo, mmiliki wa nyumba ambaye ana taarifa za kizazi kutokea, mtu yeyote ambaye amekuwapo wakati kizazi kikitokea au mtu yeyote ambaye mtoto aliyezaliwa yuko katika himaya yake ana wajibu kusajili kizazi.

### 3.0 UMUHIMU WA CHETI CHA KUZALIWA

#### 3.1 Takwimu

Cheti cha kuzaliwa ni njia muhimu inatotumiwa na Serikali kupata kwa haraka

takwimu ambazo hutumika kupanga utolewaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kama vile huduma za afya na elimu.

#### 3.2 Kupata Huduma za Kijamii

Huduma nyingi za kijamii zimefungamanishwa na cheti cha kuzaliwa. Hii inajumuisha kuandikisha mtoto shule, kupata bima ya afya na kuomba mkopo kutoka Bodi ya Mkopo kwa wanafunzi wanaoijiunga na elimu ya juu.

#### 3.3 Kupata Nyaraka za kitaifa

Cheti cha kuzaliwa ni miongoni mwa nyaraka ambazo zinahitajika ili kupata hati ya kusafiria na kitambulisho cha Taifa.

#### 3.4 Hati ya Umiliki wa Ardhi

Miongoni mwa nyaraka zinazoambatishwa katika kuomba hati ya umiliki wa ardhi ni cheti cha kuzaliwa.

#### 3.5 Kuomba kazi

Cheti cha kuzaliwa pia ni miongoni mwa nyaraka zinazoambatishwa katika kuomba kwa baadhi ya nafasi za kazi.

#### 4.0 UTARATIBU WA KUSAJILI VIZAZI

Kabidhi wasii Mkuu amepewa jukumu la kusajili vizazi. Hata hivyo, sheria imempatia Kabidhi Wasii Mkuu mamlaka ya kukasimisha uandikishaji wa vizazi kwa watendaji wafuatao:

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ;  
Mtendaji wa Kata; na  
Mtendaji wa Mtaa au Kijiji.

Katika kutekeleza jukumu hili watendaji wanapokea maelekezo ya utendaji wao kutoka kwa Kabidhi Wasii Mkuu

#### 4.1 MUDA WA USAJILI

Usajili wa vizazi umegaawanyika katika makundi matatu.

Usajili wa vizazi ndani ya siku 90, usajili huu unafanyika kwa kuwasilisha tangazo la kuzaliwa.

Usajili wa vizazi baada ya siku 90, usajili huu unahusu mtoto asiye vuka umri wa miaka 10. Kiambatanisho kinachoweza kutumika ni kadi ya kliniki au cheti cha ubatizo.

Usajili wa vizazi kwa mtu ambaye amezidi miaka 10 muombaji anatakiwa kuwasilisha kadi ya kliniki, cheti cha ubatizo, kadi ya kupigia kura, kitambulisho cha Taifa, barua kutoka Serikali za mitaa iliyopitishwa na Ofisi za Kata ambayo muombaji anaihi, na kadi ya kupigia kura ya mzazi mmoja.

#### 5. 0 MAREKEBISHO YA JINA

Ikiwa mtoto amesajiliwa kabla ya kupewa jina au kuna mabadiliko katika jina alilosajiliwa, mzazi au mlezi anaweza muda wowote kabla mtoto hajatimiza 18, kubadili jina katika cheti cha kuzaliwa baada ya msajili kujiridhisha na sababu zilizotolewa.